JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

SERA YA MAENDELEO ENDELEVU YA VIWANDA YA MWAKA 2025

2025

SERA YA MAENDELEO ENDELEVU YA VIWANDA YA MWAKA 2025

2025

YALIYOMO

VIFUPISHO ii
FASIRI YA MANENO YALIYOTUMIKA ..... iii-iv
DIBAJI v
1. UTANGULIZI 1
1.1 Usuli 1
1.2 Hali Ilivyo 2
1.2.1 Uongezaji wa thamani na mnyororo wa thamani 2
1.2.2 Viwanda vya kimkakati 3
1.2.3 Upatikanaji na ufikiwaji wa soko 4
1.2.4 Utafiti na ubunifu 4
1.2.5 Masuala Mtambuka 5
2. UMUHIMU, DIRA, DHAMIRA NA MALENGO 7
2.1 Umuhimu 7
2.2 Dira, Dhamira na Malengo 8
2.2.1 Dira 8
2.2.2 Dhamira 8
2.2.3 Malengo 8
3. MASUALA YA KISERA, MALENGO NA MATAMKO 9
3.1 Uongezaji Thamani na Mnyororo wa Thamani 9
3.2 Viwanda vya Kimkakati 10
3.3 Upatikanaji na Ufikiwaji wa Soko 10
3.4 Utafiti na Ubunifu 11
3.5 Masuala Mtambuka 11
4. MFUMO WA KISHERIA 13
5. MFUMO WA KITAASISI, UFUATILIAJI NA TATHMINI 14
5.1 Mfumo wa Kitaasisi 14
5.2 Wajibu na Majukumu ya Wadau 14
5.3 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini 18
5.4 Hitimisho 18

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na 1: Wajibu na Majukumu ya Wadau 14

VIFUPISHO

AfCFTA	Eneo Huru la Biashara la Afrika
AZAKI	Asasi za Kiraia
AZISE	Asasi Zisizo za Serikali
CAMARTEC	Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini
EAC	Jumuiya ya Afrika Mashariki
EU	Umoja wa Ulaya
FCC	Tume ya Ushindani
KMTC	Kiwanda cha Kuzalisha Mashine na Mitambo cha Kilimanjaro
NFRA	Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula
SADC	Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika
SIDO	Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo
TEMDO	Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania
TIRDO	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
VVU	Virusi vya UKIMWI
WTO	Shirika la Biashara Duniani

FASIRI YA MANENO YALIYOTUMIKA

NENO	UFAFANUZI
Kiwanda (wingi viwanda)	Mahali panapofanyika shughuli za uchakataji, utengenezaji ama uunganishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuziuza
Maendeleo ya viwanda	Mafanikio ya ukuaji wa kiuchumi yanayotokana na utafiti, uundaji, majaribio ya tafiti, usambazaji wa teknolojia, mafunzo, ujenzi na uendelezaji wa viwanda
Mazingira wezeshi ya viwanda	Jitihada mbalimbali zinazofanyika ili kuchochea maendeleo ya viwanda
Mitaji	Inahusisha miundombinu wezeshi iliyopo, fedha taslimu, malighafi, wataalam, na teknolojia inayohitajika kwa ajili ya uzalishaji kiwandani
Ukuaji wa viwanda	Mchakato wa kuhama kutoka katika uchumi unaotegemea kilimo na uzalishaji wa mikono kwenda katika uzalishaji unaotegemea mashine, kupitia utafiti na ubunifu, usanifu, uendelezaji, utengenezaji, upimaji, uzingatiaji wa ubora, mauzo, na huduma za baada ya mauzo, kwa lengo la kuwa mshindani thabiti katika soko la bidhaa husika
Mnyororo wa thamani	Muunganiko wa shughuli mbalimbali za uongezaji thamani katika bidhaa au huduma kuanzia uzalishaji hadi kumfikia mlaji
Uendelezaji wa viwanda	Shughuli zinazojumuisha kutafiti, kusanifu, kuanzisha, kuzalisha bidhaa kiwandani, kupima, kuuza, kuendeleza huduma baada ya mauzo, na kuimarisha ubora wa bidhaa kwa lengo la kukuza ushindani.
Ufikiwaji wa soko	Kipimo cha kiwango ambacho bidhaa au huduma inatumiwa na watu ikilinganishwa na ukubwa wa soko linalokadiriwa kwa bidhaa au huduma hiyo.
Uongezaji thamani	Hatua katika mchakato wa uzalishaji inayoboresha bidhaa au huduma ili kuongeza thamani yake
Upatikanaji wa soko	Uwezo wa kampuni au nchi kuuza bidhaa au huduma zake ndani na nje ya nchi

Uzalishaji kiwandani	Mchakato wa kubadilisha malighafi mbalimbali kuwa bidhaa katika mazingira ya viwanda au huduma ili kuongeza thamani.
Uzalishaji wa bidhaa	Sehemu ya uzalishaji kiwandani ambayo huhusisha mchakato wa kubadilisha malighafi kuwa bidhaa kamili zinazoonekana, kwa kutumia hasa mitambo na nguvukazi katika kiwanda
Viwanda vya kimkakati	Viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumika katika kutengeneza bidhaa nyingine, kuzalisha ajira za moja kwa moja kuanzia watu 2,000, kuongeza thamani ya madini adimu, na kuzalisha bidhaa ambazo zaidi ya asilimia 80 zitauzwa nje ya nchi
Wadau	Sekta binafsi, kampuni ya umma, wabia wa maendeleo, mashirika ya kimataifa, AZAKI na AZISE wenye nia ya kushiriki ama wanaoshiriki katika maendeleo ya viwanda

DIBAJI



Mwaka 1996, Serikali ilitunga Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 iliyolenga kuwezesha nchi kufikia ukuaji endelevu wa sekta ya viwanda ili kuwezesha uzalishaji wa ajira, mageuzi ya kiuchumi, maendeleo jumuishi, viwanda mbadala kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje, na ukuzaji wa mauzo ya nje. Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 ilitoa mwongozo uliowawezesha wadau mbalimbali kushiriki katika maendeleo ya sekta ya viwanda, ikiwa ni pamoja na Serikali, watoa huduma, wawekezaji, na washirika wa maendeleo.

Katika zaidi ya miongo miwili ya utekelezaji wa Sera, kumekuwapo na ongezeko la mauzo ya nje ya bidhaa zilizozalishwa viwandani ambazo hapo awali ziliagizwa kutoka nje, mathalani saruji, marumaru, nguo na mavazi. Aidha, ajira zinazotokana na shughuli za viwanda zimeongezeka sambamba na kuongezeka kwa mchango wa sekta katika uchumi wa nchi.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa Sera, kumekuwapo na hitaji la kuifanyia marekebisho ili kuiwianisha na vipaumbele vya taifa vilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na miongozo ya mitangamano ya kikanda na kimataifa, kama vile EAC, SADC na AfCFTA, ili kuwezesha wadau wa sekta ya viwanda kutumia fursa zinazoibuka. Aidha, hitaji la marekebisho limetokana na kuwapo kwa mabadiliko ya kiteknolojia yanayoongoza shughuli za maendeleo ya viwanda kutokana na maarifa mapya yanayopaswa kuzingatiwa.

Kutokana na changamoto na fursa zilizotajwa hapo juu, kulikuwa na hitaji la kufanya marekebisho ya Sera ili kuzingatia maendeleo mapya, kutumia fursa za kikanda na kimataifa, na kutatua changamoto zilizojitokeza katika sekta. Hivyo, Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 2025 imeweka mazingira wezeshi ambayo yatachochea maendeleo ya sekta ya viwanda ili kukidhi mahitaji halisi ya wadau.

Kwa kuwa mchakato wa kuandaa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 2025 ulishirikisha wadau mbalimbali, ninatumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioshiriki na kuwezesha kazi hii kukamilika.

Wizara inatarajia kutakuwa na jitihada za pamoja kutoka kwa wadau wote wa maendeleo ya viwanda katika kuwezesha utekelezaji wa Sera hii. Ni imani yangu kuwa kupitia jitihada hizo, Sekta ya Maendeleo ya Viwanda itafikia lengo lake kuu la kuongeza mchango wake katika uchumi wa nchi. Kufikiwa kwa malengo ya Sera kutawezesha kufikiwa kwa malengo mahususi ya viwanda yalioainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

.....

Judith S. Kapinga (Mb.)
WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA

1. UTANGULIZI

1.1 USULI

Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 ilitungwa kwa lengo kuu la kuongeza kasi ya uanzishaji na uendelezaji wa viwanda Tanzania huku ikizingatia mageuzi ya kiuchumi ya kitaifa na kimataifa yaliyoibuka. Malengo mahususi yalikuwa ni kuboresha maendeleo ya watu kwa kuzalisha ajira, kuchochea mageuzi ya kiuchumi, kuboresha urari wa malipo, kuimarisha uhifadhi wa mazingira, kuwezesha maendeleo jumuishi, kukuza uwezo wa viwanda vipya, na kuimarisha viwanda mama. Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 ilijikita katika kuendeleza sekta binafsi, kuweka mazingira wezeshi, kuzingatia malengo mahususi ya kitaifa, kuzalisha ajira na kutumia rasilimali zinazopatikana ndani ya nchi, na kutoa mwongozo kuhusu majukumu ya sekta binafsi na Serikali katika maendeleo ya viwanda.

Baada ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 kwa zaidi ya miongo miwili, mafanikio kadhaa yalifikiwa, ikiwamo thamani ya bidhaa zilizotengenezwa viwandani iliongezeka kutoka shilingi milioni 254,326 mwaka 1996 hadi kufikia shilingi milioni 13,182,066 mwaka 2023; kiwango cha ukuaji wa shughuli za uzalishaji viwandani kwa mwaka kiliongezeka kutoka asilimia 4.8 mwaka 1996 hadi kufikia asilimia 5.8 mwaka 2019; na mchango wa sekta ya viwanda katika pato la taifa uliongezeka kutoka asilimia 1.1 mwaka 1996 hadi kufikia asilimia 7.0 mwaka 2023.

Mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa ajira katika sekta rasmi ya viwanda vyenye wafanyakazi zaidi ya kumi, ambapo idadi ya wafanyakazi iliongezeka kutoka 63,317 mwaka 1999 hadi kufikia wafanyakazi 374,485 mwaka 2022; thamani ya mauzo ya bidhaa za viwanda iliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 30.1 mwaka 1999 hadi kufikia dola za Marekani milioni 91,419.2 mwaka 2022; na thamani ya mauzo ya bidhaa za viwanda zilizouzwa nje iliongezeka kutoka dola za Marekani milioni 902.7 mwaka 1996 hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,363.3 kwa mwaka 2023.

Licha ya mafanikio yaliyotajwa hapo juu, sekta ya Maendeleo ya Viwanda inakabiliwa na changamoto za kisera ambazo zinahitaji kushughulikiwa ili kuongeza kasi ya maendeleo ya viwanda. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kumalizika kwa kipindi cha utekelezaji wa Sera, ambapo baadhi ya malengo hayajakamilika na yanahitaji kuhuishwa; kuwepo kwa masuala kadhaa yanayoibuka, kama vile maendeleo ya teknolojia za viwanda; usanifu wa Sera kujumuisha masuala ya sekta nyingine, kama vile sera za fedha na kodi ambazo sekta haiwezi kuzishughulikia kikamilifu; na kuongezeka kwa uhuria wa uchumi hususan kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika maendeleo ya viwanda, ambako kunahitaji mwongozo wa kisera.

Changamoto nyingine ni pamoja na hitaji la kuzingatia mwongozo wa Serikali wa uandaaji wa Sera; kumalizika kwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na uwepo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, ambapo Sera ya Maendeleo ya Viwanda ni mojawapo ya nyenzo za utekelezaji; na maendeleo ya mtangamano wa kiuchumi wa kikanda na kimataifa kama vile kuridhia Itifaki ya Viwanda ya SADC, ambayo inahitaji nchi wanachama kuwianisha sera zao za maendeleo ya viwanda na nyaraka hizo. Kutokana na changamoto hizo za kisera, Serikali ilipaswa kufanya marekebisho ya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 ili kutoa mwongozo mpya wa maendeleo ya viwanda.

1.2 HALI ILIVYO

Wakati wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020, malengo mahususi yalikuwa ni kuboresha maendeleo ya watu kwa kuzalisha ajira, kuchochea mageuzi ya kiuchumi, kuboresha urari wa malipo, kuimarisha uhifadhi wa mazingira, kuwezesha maendeleo jumuishi, kukuza uwezo wa viwanda vipya, na kuimarisha viwanda mama. Hali ya utekelezaji wa Sera imefafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

1.2.1 Uongezaji wa thamani na mnyororo wa thamani

Tanzania ina rasilimali za aina mbalimbali kama vile, mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, madini na misitu zinazopatikana nchini kote. Ili kutumia fursa zitokanazo na maliasili hizo, Serikali kwa kushirikiana na wadau, walianzisha na kutekeleza mikakati na mipango kadhaa ikiwamo Mkakati Unganishi wa Maendeleo ya Viwanda 2011–2025, Mkakati wa Maendeleo ya Alizeti 2016–2020, Mkakati wa Maendeleo ya Ngozi 2016–2020, Mkakati wa Maendeleo wa Nguo kutoka kwenye Pamba 2016–2020, Mkakati wa Kuendeleza Mazao ya Jamii ya Kunde 2016-2020, Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (Awamu I na II), na kutungwa kwa sheria mbalimbali.

Pamoja na mikakati na mipango hiyo, jitihada zingine zilizofanyika ni kuanzisha na kuboresha utendaji wa taasisi zinazosaidia uongezaji wa thamani wa rasilimali, kama vile Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania, Bodi ya Tumbaku Tanzania, Bodi ya Sukari Tanzania, Bodi ya Pamba Tanzania, Bodi ya Korosho Tanzania, Bodi ya Kahawa Tanzania, Bodi ya Nyama Tanzania, Bodi ya Maziwa Tanzania, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC), Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO), Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), Tume ya Madini Tanzania, na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Taasisi hizi zilianzishwa ili kuwa na mchango katika kusimamia mnyororo wa thamani na ongezeko la thamani la mazao mbalimbali.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili la sera ni pamoja na kuanzishwa kwa viwanda nane (8) vya nguo na mavazi ambavyo kwa mwaka vinasokota tani 36,742; kusuka mita milioni 145; kufuma tani 7,920; na kutengeneza nguo na mavazi milioni 43. Aidha, viwanda vitatu (3) vya sukari vilianzishwa na vinne (4) viliboreshwa. Viwanda hivyo vina uwezo wa kuzalisha jumla ya tani 460,200 za sukari kwa mwaka. Vilevile, viwanda 11 vya saruji vilianzishwa na vitatu (3) viliboreshwa ambavyo kwa jumla vinaweza kuzalisha wastani wa tani 9,107,973 za saruji kwa mwaka. Pia, viwanda mbalimbali vilianzishwa, vikiwamo viwili (2) vya marumaru vinavyotengeneza mita za mraba milioni 18 kwa mwaka; viwanda 23 vya mbolea; viwanda tisa (9) vya usindikaji wa ngozi, vyenye uwezo wa kusindika vipande milioni 2.5 kwa mwaka; viwanda 16 vya usindikaji wa samaki; viwanda 17 vya kuzalisha mafuta ya kula; na viwanda vinne (4) vya vioo vinavyotengeneza tani 292,800 za vioo kwa mwaka.

Licha ya mafanikio hayo, Tanzania bado inauza kiasi kidogo cha bidhaa zilizoongezwa thamani. Aidha, kuna hasara zitokanazo na kukosekana kwa ufanisi katika uongezaji thamani wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, madini na misitu.

Hali hii inasababishwa na upungufu wa wataalamu wenye ujuzi, miundombinu wezeshi kwa maendeleo ya viwanda vya uongezaji thamani na mnyororo wa thamani isiyotosheleza, na upungufu wa mitaji. Hivyo, ili kukabiliana na changamoto hizo ipasavyo, msukumo mpya wa kisera unahitajika.

1.2.2. Viwanda vya kimkakati

Viwanda vya kimkakati huzalisha bidhaa zinazotumika katika utengenezaji wa bidhaa nyingine. Pia, huchangia kwa kiasi kikubwa katika uzalishaji wa ajira na bidhaa za kuuza nje na uongezaji thamani kwenye madini adimu. Viwanda vya kimkakati ni pamoja na viwanda vya uundaji na utengenezaji wa mashine na mitambo, uzalishaji wa kemikali, uzalishaji wa mikrochipu, uongezaji thamani kwenye madini adimu, utengenezaji wa nguo na mavazi, uundaji na utengenezaji wa vifaa vya ulinzi, na uundaji na utengenezaji wa magari. Ili kukuza uanzishwaji wa viwanda vya kimkakati, Serikali ilirekebisha na kuboresha ufanisi wa Kiwanda cha Kuzalisha Mashine na Mitambo cha Kilimanjaro (KMTC) kwa kuimarisha uwezo wake wa kutengeneza mashine za kuchakata mazao ya misitu, kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo, na kutengeneza vipuri muhimu kwa ajili ya mashine za uchimbaji madini na ujenzi. Jitihada zingine ni ukamilishaji wa utekelezaji wa mradi unganishi wa kuzalisha chuma wa Mchuchuma na Liganga na mradi wa kuzalisha magadisoda wa Engaruka.

Aidha, ukarabati wa vituo sita (6) vya kuendeleza teknolojia vya SIDO na karakana ya TEMDO ulifanyika. Ukarabati huo ulihusisha usimikaji wa mashine za kisasa kwa ajili ya utengenezaji wa mitambo inayotumika katika shughuli za kilimo, ujenzi na uchakataji wa madini. Vilevile, jumla ya viwanda 13 vya kuunganisha magari vilianzishwa, ambapo viwanda 11 ni vya kuunganisha matela ya kusafirishia mizigo na viwili (2) ni vya kuunganisha magari ya kubeba mizigo, ikiwa ni pamoja na malori na matipa. Kwa upande wa viwanda, vinavyohitaji nguvukazi nyingi viwanda nane (8) vya nguo na mavazi vilianzishwa, vikizalisha ajira za moja kwa moja 15,300 na zisizo za moja kwa moja 45,000.

Licha ya mafanikio yaliyobainishwa hapo juu, bado kuna fursa ambazo hazijatumika katika maeneo mbalimbali kama vile uchimbaji na uchakataji wa chuma ghafi na chuma cha pua, uundaji na utengenezaji wa mashine na mitambo, uundaji na uunganishaji wa magari, uzalishaji wa kemikali, utengenezaji wa dawa za binadamu na vifaa tiba, uundaji na utengenezaji wa vifaa vya uzalishaji wa nishati, uundaji na utengenezaji wa vifaa vya ulinzi na uzalishaji wa chipu. Maeneo mengine yenye fursa nyingi ni uzalishaji wa mitambo na vifaa vya elektroniki na mawasiliano; uzalishaji wa mitambo inayotumia akili unde; na uzalishaji wa zana za kilimo na mitambo ya uchakataji wa mazao ya kilimo, uvuvi, mifugo na na misitu; na uzalishaji wa nguo na mavazi pamoja na ngozi na bidhaa za ngozi.

Pia, viwanda vya kimkakati vilivyopo nchini vinatumia teknolojia za zamani, na hivyo kuzalisha bidhaa ambazo haziwezi kushindana na bidhaa za aina hiyo zinazozalishwa katika nchi zilizoendelea kiteknolojia. Hali hii inasababisha nchi kutegemea zaidi kuagiza vipuri, mashine, madawa ya binadamu na mifugo; na bidhaa za kati kutoka nje. Hivyo, marekebisho ya Sera yanahitajika ili kukabiliana na changamoto hizo.

1.2.3 Upatikanaji na ufikiwaji wa soko

Katika kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa soko la bidhaa za viwandani, Serikali imefanya jitihada mbalimbali zinazolenga masoko ya ndani na ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uuzaji wa bidhaa zilizoongezwa thamani na kuboresha njia za usambazaji za ndani, kikanda na kimataifa. Kuhusu soko la ndani, jitihada muhimu zilizofanywa ni pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya viwanda na masoko ya ndani, kuboresha miundombinu ya masoko, kuimarisha minyororo ya usambazaji kwa wazalishaji wa ndani, kuanzisha maeneo ya viwanda, na kuandaa maonesho ya biashara.

Katika soko la kimataifa, Serikali imefanya jitihada za kuimarisha ujumuishaji wa biashara kupitia makubaliano baina ya nchi, ya kikanda na ya kimataifa. Ili kutekeleza makubaliano hayo, Serikali imeridhia itifaki na kuingia mikataba mbalimbali katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA), na Shirika la Biashara Duniani (WTO). Itifaki zilizoridhiwa ni pamoja na Itifaki ya Soko la Pamoja la EAC; Itifaki ya Umoja wa Forodha wa EAC; Itifaki ya EAC ya Afya na Usafi wa Chakula (SPS); na Itifaki ya Viwango, Uthibiti Ubora na Vipimo. Kupitia mtangamano wa kibiashara, katika mwaka 2023, mauzo ya nje ya nchi yalifikia dola za Marekani milioni 1,414.9 kwa soko la EAC, dola za Marekani milioni 1,727.5 kwa soko la SADC, dola za Marekani milioni 1,498.3 kwa soko la Umoja wa Ulaya (EU), dola za Marekani milioni 2,924.1 kwa soko la Asia, na dola za Marekani milioni 80.4 kwa soko la Marekani.

Licha ya mafanikio yaliyotajwa hapo juu, nchi inaagiza zaidi bidhaa zilizozalishwa viwandani kuliko inavyouza katika masoko ya nje. Hali hii inachangiwa na masuala kadhaa, ikiwa ni pamoja na uhaba wa ujuzi wa masoko, hususani kwenye eneo la majadiliano ya kibiashara, na miundombinu ya masoko isiyotosheleza. Changamoto zingine ni wazalishaji kutozingatia viwango vya soko; uwezo mdogo wa kutumia fursa za upendeleo zinazotokana na makubaliano ya mitangamano; na kushindwa kufikisha bidhaa kwa walaji kwa wakati. Hivyo, ili kukabiliana na changamoto hizo ipasavyo, msukumo mpya wa kisera unahitajika.

1.2.4 Utafiti na ubunifu

Utafiti na ubunifu katika maendeleo ya viwanda unahusisha ubunifu wa mawazo mapya yanayowezesha uundaji wa teknolojia mpya, mifumo ama uboreshaji wa teknolojia iliyopo na kwa matumizi ya viwandani na kuisambaza ili kuimarisha na kuboresha uzalishaji wa bidhaa za viwandani. Utafiti na ubunifu una mchango mkubwa katika uchumi wa kisasa kutokana na ongezeko la maarifa mapya na matumizi yake. Katika kufanikisha shughuli za utafiti na ubunifu, Serikali imeimarisha utendaji wa taasisi mbalimbali zikiwamo TEMDO; CAMARTEC; TIRDO; vyuo vikuu vya umma na binafsi; na taasisi za utafiti wa kilimo, mifugo na uvuvi. Kupitia jitihada hizo, mafaniko mbalimbali yamejitokeza, ambapo teknolojia 620 zilizobuniwa na taasisi hizo zimesambazwa na zinaendelea kutumika. Vilevile, programu 12 za viatamizi zilianzishwa ili kuwasaidia wabunifu kuendeleza teknolojia zao na kuzifanya zitumike kibiashara.

Licha ya jitihada zilizofanywa na Serikali, utafiti na ubunifu bado ni wa kiwango cha chini. Hali hii inasababishwa na upungufu wa miundombinu ya utafiti na ubunifu, uwekezaji mdogo katika utafiti na ubunifu, motisha kidogo kwa watafiti, uchache wa watafiti, kutokwenda na kasi ya mabadiliko ya teknolojia, na kukosekana kwa muunganiko kati ya viwanda na taasisi za utafiti. Hivyo, marekebisho ya Sera yanahitajika.

1.2.5 Masuala Mtambuka

1.2.5.1 Wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu

Tanzania ina nguvukazi ya watu 25,861,023 ambapo asilimia nne (4) ndio wanaopata nafasi ya kuajiriwa viwandani. Ufinyu huo wa ajira unaleta changamoto zaidi kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kuinua na kutumia vipaji vya ujasiriamali miongoni mwa makundi maalumu ili kuwajumuisha kwenye sekta ya viwanda ni muhimu katika kuendeleza makundi haya. Mahitaji ya msingi ya kujenga ushiriki wenye ufanisi wa makundi maalumu kwenye sekta ni kutambua mahitaji yao maalumu katika ngazi tofauti za viwanda, kuanzia uanzishwaji hadi ukuaji wake, na kuyajumuisha kwenye Sera. Serikali kwa kushirikiana na wadau wa viwanda inaendeleza jitihada za kujumuisha masuala ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika maendeleo ya viwanda. Hivyo, marekebisho ya Sera yataongeza msukumo wa ushirikishwaji wa makundi hayo maalumu.

1.2.5.2 Uhifadhi wa mazingira

Maendeleo ya sekta ya viwanda nchini ni muhimu katika ukuaji wa Uchumi, ingawa viwanda vinaweza kuchangia kufanya uchafuzi wa mazingira ambao una athari hasi kwa afya ya binadamu na mazingira. Mathalani, uchafuzi wa mazingira utokanao na gesi ya ukaa nchini Tanzania uliongezeka kutoka 435.30 Gg mwaka 1996 mpaka kufikia 696.58 Gg mwaka 2005 na kuchangia kuongeza madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi katika dunia. Serikali imechukua hatua mbalimbali za kulinda na kuhifadhi mazingira katika sekta ya viwanda, zikiwamo kuanzishwa kwa mfumo wa kisheria na kitaasisi wa uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Licha ya jitihada hizo, sekta bado inakabiliwa na changamoto za uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za viwanda zisizozingatia utumiaji wa teknolojia rafiki kwa mazingira. Hivyo, jamii inahitaji elimu zaidi kuhusu hatua za kuchukua ili kulinda mazingira kutokana shughuli za maendeleo ya viwanda, ambazo zinatakiwa kujumuishwa katika Sera kwa kuwajengea uwezo wenye viwanda.

1.2.5.3 VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa

Shughuli za viwanda hukutanisha makundi makubwa na tofauti ya watu zikihusisha wafanyakazi, watoa huduma, na wadau wengine ambao mwingiliano wao wa mara kwa mara unaweza kuongeza hatari ya kuenea kwa VVU/UKIMWI. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imefanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na VVU/UKIMWI katika shughuli za viwanda. Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika ili kujenga uelewa wa wadau kuhusu masuala ya VVU/UKIMWI.

Aidha, shughuli za viwanda husababisha watu kupata msongo wa mawazo, sonona na ulaji usiozingatia kanuni za afya, kutopumzika vya kutosha na hivyo kuwa katika hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukizwa kama vile shinikizo la damu, kisukari, magonjwa ya moyo na figo. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imefanya jitihada za kukabiliana na magonjwa yasiyoambukizwa katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya viwanda. Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika ili kujenga uelewa wa wadau kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa.

2. UMUHIMU, DIRA, DHAMIRA NA MALENGO

2.1 UMUHIMU

Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 imekuwa ikitekelezwa kwa zaidi ya miongo miwili. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kuna masuala muhimu yaliyolazimu kufanya marekebisho ya Sera hiyo kama yalivyobainishwa hapa chini.

i. **Kuwezesha Sekta Kuhimili Mabadiliko:** Tangu kutungwa kwa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020, kumetokea mabadiliko makubwa ya kitaifa na kimataifa katika maendeleo ya viwanda, hususani uvumbuzi na matumizi ya teknolojia kama vile akili unde, mikrochipu na roboti ambazo hazikuzingatiwa katika Sera inayorejewa.

ii. **Kutumia Fursa za Mtangamano wa Kikanda na Kimataifa:** Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera, kumekuwapo na makubaliano mbalimbali katika mtangamano wa kikanda na kimataifa kama vile kuingiwa kwa mikataba na kuridhiwa kwa itifaki mbalimbali zinazohusu maendeleo ya viwanda katika SADC, AfCFTA, na EAC. Hali hii inaleta ulazima wa kuwa na sera na mipango inayowiana. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 ilifanyiwa marekebisho.

iii. **Kuwianisha Sera na Vipaumbele vya Kitaifa:** Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 imekuwa mojawapo ya nyenzo muhimu za kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambayo kwa sasa inafikia ukomo na hivyo kutoa nafasi ya kuandaliwa kwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Dira hiyo inalenga kujenga uchumi unaoongozwa na ujenzi na uendelezaji ya viwanda. Hivyo, Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 inafanyiwa marekebisho ili kuwezesha utekelezaji wa masuala ya maendeleo ya viwanda yaliyobainishwa katika Dira 2050.

iv. **Kuboresha Muundo wa Uendeshaji wa Sekta ya Viwanda:** Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera kumejitokeza mabadiliko makubwa yaliyotokana na kubadilika kwa muundo na mbinu za uzalishaji na mifumo ya uongezaji thamani kimataifa. Masuala haya yalihitaji mwongozo wa kisera ili kuboresha muundo wa uendeshaji wa sekta na kuwezesha ushiriki thabiti wa sekta binafsi katika maendeleo ya uchumi.

v. **Kuondoa Majukumu Yanayoratibiwa na Sera Nyingine za Kisekta:** Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 ilijumuisha majukumu yanayoratibiwa na sekta nyingine kama vile majukumu ya sera za fedha na kodi. Jambo hili linaleta mkanganyiko katika utekelezaji na ufuatiliaji wa malengo ya Sera. Marekebisho yanalenga kufanya usanifu mpya wa Sera ili kujikita zaidi katika masuala ya maendeleo ya viwanda yanayotekelezwa na kutolewa taarifa na Wizara yenye dhamana.

vi. **Kukoma kwa Muda wa Sera na Kukamilika kwa Baadhi ya Malengo:** Usanifu wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya 1996–2020 ulihusisha ukomo wa kipindi cha utekelezaji ambao hauendani na usanifu unaoelekezwa na mwongozo wa uandishi wa Sera. Hali hii imesababisha baadhi ya malengo ya Sera kukamilika kama vile lengo la kurekebisha muundo wa umiliki wa viwanda na malengo mengine kutokamilika katika kipindi kilichobainishwa. Kutokana na hoja hizo, Sera hii ilihitaji kufanyiwa marekebisho ili kuhuisha malengo.

2.2 DIRA, DHAMIRA NA MALENGO

2.2.1 Dira

Kuwa na uchumi shindani, endelevu na jumuishi unaoongozwa na maendeleo ya viwanda.

2.2.2 Dhamira

Kuhamasisha maendeleo endelevu ya viwanda kwa kuongeza thamani ya malighafi na kuboresha minyororo ya thamani; kuwekeza kwenye utafiti na ubunifu; na kuendeleza viwanda vya kimkakati.

2.2.3 Malengo

Lengo Kuu

Kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika maendeleo ya uchumi wa nchi.

Malengo mahususi

Malengo mahususi ya Sera hii ni:

i. Kuimarisha uongezaji thamani na mnyororo wa thamani katika mazao na rasilimali nyingine;
ii. Kuanzisha na kuimarisha viwanda vya kimkakati;
iii. Kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa soko la bidhaa zilizozalishwa viwandani ndani na nje ya nchi;
iv. Kuwezesha utafiti na ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya viwanda; na
v. Kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za uendelezaji viwanda.

3. MASUALA YA KISERA, MALENGO NA MATAMKO

Sura hii inahusu masuala ya kisera, malengo ya Sera na matamko ya kisera kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

3.1 UONGEZAJI THAMANI NA MNYORORO WA THAMANI

Tanzania ina rasilimali za aina mbalimbali zinazopatikana nchini kote kama vile mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, madini na mazao ya misitu. Ili kutumia fursa zilizopo, Serikali ilianzisha na kutekeleza mikakati na mipango kadhaa, ikiwamo Mkakati Unganishi wa Maendeleo ya Viwanda wa mwaka 2011–2025; Mkakati wa Maendeleo wa Alizeti 2016–2020; na Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Ngozi 2016–2020. Jitihada nyingine ni kuanzisha taasisi zinazosaidia uongezaji wa thamani.

Licha ya jitihada hizo, Tanzania bado inauza nje kiasi kidogo cha bidhaa zilizoongezwa thamani. Aidha, kuna hasara zitokanazo na kukosekana kwa ufanisi katika uongezaji thamani wa mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, madini na misitu. Hali hii inasababishwa na upungufu wa wataalamu wenye ujuzi; miundombinu wezeshi kwa maendeleo ya viwanda vya uongezaji thamani na mnyororo wa thamani isiyotosheleza; na upungufu wa mitaji.

Lengo

Kuimarisha uongezaji thamani na mnyororo wa thamani katika mazao na rasilimali nyingine

Matamko

Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha:

i. Bidhaa zinazotokana na mazao na rasilimali nyingine zinaongezewa thamani;
ii. Fedha kwa ajili ya maendeleo ya viwanda zinapatikana kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda na vyanzo vingine;
iii. Kunakuwa na miundombinu ya maendeleo ya viwanda inayotosheleza;
iv. Kunakuwa na wataalamu wenye ujuzi katika mnyororo wa uongezaji thamani; na
v. Mitaji iliyowekezwa katika shughuli za maendeleo ya viwanda inalindwa kwa kuwekewa bima.

3.2 VIWANDA VYA KIMKAKATI

Viwanda vya kimkakati ni pamoja na viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumika katika utengenezaji wa bidhaa nyingine na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uzalishaji wa ajira, bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje, na kuongeza thamani kwenye madini adimu. Viwanda vya kimkakati ni pamoja na viwanda vya uundaji na utengenezaji wa mashine na mitambo, uzalishaji wa kemikali muhimu, uzalishaji wa mikrochipu, uongezaji thamani kwenye madini adimu, utengenezaji wa nguo na mavazi, uundaji na utengenezaji wa vifaa vya ulinzi, uundaji na utengenezaji wa magari.

Tanzania ina rasilimali za madini, yakiwemo ya chuma, nikeli na grafiti; hata hivyo, mahitaji ya mashine, mitambo, magari, kemikali; dawa za binadamu na vifaa tiba; vifaa vya kuzalishia nishati; vifaa vya elektroniki na mawasiliano, uundaji na utengenezaji wa vifaa vya ulinzi na uzalishaji wa chipu na akili unde; zana za kilimo; uchakataji wa mazao ya kilimo na mifugo; uzalishaji wa nguo na mavazi pamoja na ngozi na bidhaa za ngozi yanatimizwa kwa kiasi kikubwa kwa kuagiza bidhaa husika kutoka nje ya nchi. Hata hivyo, viwanda vya kimkakati vilivyopo vinatumia teknolojia iliyopitwa na wakati na vinakabiliwa na upungufu wa mitaji na miundombinu wezeshi. Hivyo, huzalisha bidhaa ambazo hazihimili ushindani na bidhaa za aina hiyo zinazozalishwa katika nchi zilizoendelea kiteknolojia. Hali hii inasababisha nchi kutegemea zaidi kuagiza mashine, mitambo, vipuri, dawa za binadamu, vifaa tiba, vifaa vya ulinzi, vifaa vya mawasiliano, kemikali muhimu na zana kilimo kutoka nje.

Lengo
Kuanzisha na kuimarisha viwanda vya kimkakati

Matamko
Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha:
i. Inaanzisha viwanda vya kimkakati katika maeneo yenye fursa za uzalishaji;
ii. Inaendeleza na kuboresha utendaji wa viwanda vya kimkakati; na
iii. Inafanya utafiti wa kina wa kubaini rasilimali za kutumika katika viwanda vya kimkakati.

3.3 UPATIKANAJI NA UFIKIWAJI WA SOKO
Katika kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa soko la bidhaa za viwandani, Serikali imefanya jitihada mbalimbali zinazolenga masoko ya ndani, pande mbili, kikanda na kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uuzaji wa bidhaa zilizoongezwa thamani na kuboresha njia za usambazaji za ndani, pande mbili, kikanda na kimataifa. Vilevile, Serikali imefanya juhudi za mtangamano wa biashara kupitia kusaini, kuridhia na kutekeleza Mikataba na Itifaki mbalimbali zinazojumuisha pande mbili, kikanda na kimataifa.

Licha ya mafanikio yaliyotajwa hapo juu, bado nchi inaendelea kuagiza bidhaa nyingi zilizozalishwa viwandani zaidi kuliko inavyouza kwenye masoko ya nje. Hali hii inachangiwa na masuala kadhaa, yakiwemo upungufu wa ujuzi wa masoko kwa bidhaa zinazozalishwa na miundombinu duni ya masoko. Changamoto nyingine ni pamoja na kushindwa kwa wazalishaji kukidhi viwango vya kimataifa, uwezo mdogo wa uzalishaji, uwezo mdogo wa kukidhi usambazaji, na uwezo mdogo wa kutumia fursa za upendeleo zinazotokana na makubaliano ya pande mbili, kikanda na kimataifa.

Lengo
Kuwezesha upatikanaji na ufikiwaji wa soko la bidhaa zilizozalishwa viwandani ndani na nje ya nchi.

Matamko
Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha:
i. Kiwango cha mauzo ya bidhaa katika soko la ndani na nje kinaongezeka;
ii. Inaanzisha na kuendeleza miundombinu ya masoko;
iii. Bidhaa zinazozalishwa zinakidhi viwango vya soko; na
iv. Inatumia kikamilifu fursa zinazotokana na makubaliano ya mitangamano katika masuala ya viwanda.

3.4 UTAFITI NA UBUNIFU
Utafiti na ubunifu unawezesha upatikanaji wa teknolojia stahiki na mifumo yake kwa ajili ya maendeleo ya viwanda. Teknolojia stahiki inaweza kuzalishwa ama kupokelewa ili kuboresha shughuli za uzalishaji viwandani. Katika kufanikisha shughuli za utafiti na ubunifu, Serikali imeimarisha utendaji wa taasisi mbalimbali zikiwamo TEMDO, CAMARTEC, TIRDO, vyuo vikuu vya umma na binafsi, na taasisi za utafiti wa kilimo, uvuvi na mifugo. Aidha, sekta binafsi pia hufanya shughuli za utafiti na ubunifu kupitia tafiti mbalimbali kwa ajili ya kuboresha uzalishaji viwandani.

Licha ya jitihada zilizofanywa na Serikali, pamoja na wadau, utafiti na ubunifu bado ni wa kiwango cha chini. Hali hii inasababishwa na upungufu wa miundombinu ya utafiti na ubunifu, uwekezaji mdogo katika utafiti na ubunifu, motisha kidogo kwa watafiti, uchache wa watafiti, kutokwenda na kasi ya mabadiliko ya teknolojia, na kukosekana kwa muunganiko kati ya viwanda na taasisi za utafiti.

Lengo
Kuwezesha utafiti na ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya viwanda

Matamko
Serikali kwa kushirikiana na wadau itahakikisha:
i. Inawezesha shughuli za ubunifu na utafiti wa maendeleo ya viwanda; na
ii. Matokeo ya utafiti yanatumika kuboresha maendeleo ya viwanda.

3.5 MASUALA MTAMBUKA
Masuala mtambuka katika Sera hii yanahusisha masuala ya uhifadhi wa mazingira; utawala bora; jinsia, vijana, na watu wenye ulemavu; VVU/UKIMWI; na magonjwa yasiyoambukizwa. Tanzania ina vijana na wanawake wanaofaa kuingia katika soko la ajira baada ya kuhitimu mafunzo kila mwaka, ingawa ni wachache wanaoweza kuingia katika soko rasmi la ajira. Kuinua na kutumia vipaji vya ujasiriamali miongoni mwa makundi maalumu ili kuwajumuisha kwenye sekta ya viwanda ni muhimu katika kuendeleza makundi haya. Mahitaji ya msingi ya kujenga ushiriki wenye ufanisi wa makundi maalumu kwenye sekta ni kutambua mahitaji yao maalumu katika ngazi tofauti za viwanda, kuanzia uanzishwaji hadi ukuaji wake, na kuyajumuisha kwenye Sera. Serikali, kwa kushirikiana na wadau wa viwanda, inaendeleza jitihada za kujumuisha masuala ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika maendeleo ya viwanda.

Maendeleo ya sekta ya viwanda nchini ni muhimu katika ukuaji wa uchumi ingawa viwanda vinaweza kuchangia kuleta athari hasi kwa mazingira. Serikali imechukua hatua mbalimbali za kulinda na kuhifadhi mazingira katika sekta ya viwanda, zikiwamo kuanzishwa kwa mfumo wa kisheria na kitaasisi wa uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Licha ya jitihada hizo, sekta bado inakabiliwa na changamoto za uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za viwanda zisizozingatia utumiaji wa teknolojia rafiki kwa mazingira. Hivyo, jamii inahitaji elimu zaidi kuhusu hatua za kuchukua ili kulinda mazingira kutokana shughuli za maendeleo ya viwanda ambazo zinahitaji kujumuishwa katika Sera kwa kuwajengea uwezo wenye viwanda. Sera iliyorekebishwa imezingatia masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira katika shughuli za maendeleo ya viwanda.

Shughuli za viwanda hukutanisha makundi makubwa na tofauti ya watu, wafanyakazi, watoa huduma, na wadau wengine ambao mwingiliano wao wa mara kwa mara unaweza kuongeza hatari ya kuenea kwa VVU/UKIMWI. Serikali kwa kushirikiana na wadau imefanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na VVU/UKIMWI katika shughuli za viwanda. Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika ili kujenga uelewa wa wadau kuhusu masuala ya VVU/UKIMWI.

Aidha, shughuli za viwanda huweza kusababisha watu kupata msongo wa mawazo, sonona, kuwa na ulaji usiozingatia kanuni za afya, kutopumzika vya kutosha na hivyo kuwa katika hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukizwa kama vile shinikizo la damu, kisukari, magonjwa ya moyo na figo. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imefanya jitihada za kukabiliana na magonjwa yasiyoambukizwa katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya viwanda. Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika ili kujenga uelewa wa wadau kuhusu magonjwa yasiyoambukizwa.

Utawala bora ni msingi muhimu katika uendelezaji wa viwanda kwa kuwa sekta hii inahusisha masuala mbalimbali, ikiwamo ajira, ambayo yanahitaji uzingatiwaji wa maadili. Jitihada mbalimbali zimefanyika za uzingatiwaji wa kanuni za utawala bora kwa kutoa mafunzo kwa wamiliki wa viwanda. Pamoja na jitihada hizo, bado kuna changamoto za uzingatiwaji wa maadili kama vile taratibu za masuala ya ajira.

Lengo
Kujumuisha masuala mtambuka katika shughuli za uendelezaji viwanda

Matamko
Serikali kwa kushirikiana na wadau itajumuisha masuala ya:
i. Utunzaji mazingira katika shughuli za uendelezaji viwanda;
ii. Wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu katika shughuli za uendelezaji viwanda;
iii. VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza katika shughuli za uendelezaji viwanda; na
iv. Utawala bora katika shughuli za uendelezaji viwanda.

4. MFUMO WA KISHERIA

Kuwapo kwa mfumo madhubuti wa kisheria ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya viwanda nchini. Kwa sasa, mfumo wa kisheria unaosimamia sekta ya viwanda unatekelezwa kupitia sheria zilizo chini ya Wizara, ambazo ni Sheria ya Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania, Sura ya 176, inayotoa maelekezo kuhusu huduma za uhandisi na usanifu viwandani na suluhisho la utengenezaji wa mashine na vifaa na kuchochea ubunifu wa kiteknolojia kwa ukuaji wa viwanda; Sheria ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda, Sura ya 159, kuhusu utafiti, kukuza maendeleo ya teknolojia, kutoa huduma za ushauri na kuwezesha ubunifu katika sekta ya viwanda; Sheria ya Taifa ya Usajili na Leseni za Viwanda, Sura ya 46, ambayo inaweka utaratibu wa kusajili viwanda nchini; na Sheria ya Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini, Sura ya 181, inayolenga kukuza matumizi ya mashine katika kilimo na teknolojia za vijijini ili kuongeza tija, uendelevu na ustawi vijijini.

Mifumo mingine ni Sheria ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, Sura ya 112, inayolenga kukuza viwanda vidogo kwa kutoa mafunzo, mitaji, utafutaji masoko, na uhawilishaji wa teknolojia; Sheria ya Shirika la Viwango la Tanzania, Sura ya 130, inayoweka na kusimamia viwango, kudhibiti ubora, kupima na kutoa vyeti vya ithibati ili kukuza ushindani wa viwanda na kulinda walaji; Sheria ya Ushindani, Sura ya 285, inayokuza ushindani na kulinda walaji dhidi ya vitendo visivyo vya haki; Sheria ya Ushindani Sura ya 285, iliyoanzisha Baraza la Ushindani linalosikiliza rufaa na kupitia maamuzi yaliyofanywa na Tume ya Ushindani (FCC); na Sheria ya Vipimo, Sura ya 340, inayosimamia, kuthibitisha, na kuhakiki usahihi wa vipimo vinavyotumika katika biashara ili kulinda walaji na biashara.

Aidha, kuna sheria nyingine za kitaifa zinazolenga kukuza maendeleo ya sekta ya viwanda nchini, ambazo ni Sheria ya Afya na Usalama Kazini, Sura ya 297; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191; Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi, Sura ya 213; Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366; na Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438. Ili kutoa mwongozo sahihi wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 2025, Serikali itapitia Sheria zilizopo na pale itakapobidi itarekebisha na kutunga Sheria mahususi ya maendeleo ya viwanda.

5. MFUMO WA KITAASISI, UFUATILIAJI NA TATHMINI

5.1 MFUMO WA KITAASISI

Wadau wakuu katika utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 2025 ni Wizara yenye dhamana ya Viwanda; Wizara za kisekta, Taasisi za Serikali zilizo chini ya Wizara za kisekta; Sekretarieti za Mikoa; na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wadau wengine ni Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Elimu na Utafiti, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Asasi Zisizo za Serikali.

5.2 WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU

Majukumu na wajibu wa wadau katika utekelezaji wa Sera yameainishwa kwenye Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 1: Wajibu na Majukumu ya Wadau

Na.	Jina la Mdau	Wajibu na Majukumu
1.	Wizara yenye dhamana ya Viwanda	Kutekeleza na kuratibu utekelezaji wa Sera na mkakati ili kuendeleza sekta ya viwanda
2.	Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	Kutoa mwongozo kuhusu miundo ya taasisi na masuala yanayohusiana na rasilimali watu
3.	Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji	Kuhakikisha kuwapo kwa mazingira rafiki na miundombinu wezeshi inayovutia uwekezaji wa viwanda
4.	Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)	Kuratibu shughuli za maendeleo ya viwanda katika ngazi za mikoa na Serikali za mitaa
5.	Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira	Kuhifadhi na kusimamia mazingira kwa ajili ya maendeleo ya viwanda
6.	Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu	Kuratibu utekelezaji na ufuatiliaji wa Sera
7.	Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu	Kutoa mwongozo jumuishi wa masuala ya stahiki za rasilimali watu, usalama na afya mahali pa kazi na makundi maalumu
8.	Wizara yenye dhamana ya Fedha	Kutoa na kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali fedha na vivutio kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
9.	Wizara yenye dhamana ya Ardhi	Kuhakikisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
10.	Wizara yenye dhamana ya Kilimo	Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za mazao ya kilimo zenye ubora na za kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
11.	Wizara yenye dhamana ya Mifugo	Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za mazao ya mifugo zenye ubora na za kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
12.	Wizara yenye dhamana ya Uvuvi	Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za mazao ya uvuvi yenye ubora na za kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
13.	Wizara yenye dhamana ya Nishati	Kuhakikisha upatikanaji wa nishati ya kutosha na yenye uhakika kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
14.	Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Nje	Kuratibu diplomasia ya uendelezaji wa viwanda
15.	Wizara yenye dhamana ya Madini	Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za madini zenye ubora na za kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
16.	Wizara yenye dhamana ya Uchukuzi	Kujenga na kuendeleza miundombinu (bandari, anga na reli) ili kukidhi mahitaji ya uendelezaji wa viwanda
17.	Wizara yenye dhamana ya Ujenzi	Kujenga na kuendeleza miundombinu ya barabara ili kukidhi mahitaji ya uendelezaji wa viwanda.
18.	Wizara yenye dhamana ya Maji	Kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda

Na.	Jina la Mdau	Wajibu na Majukumu
19.	Wizara yenye dhamana ya Mawasiliano	Kuhakikisha upatikanaji wa miundombinu ya mawasiliano kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
20.	Wizara yenye dhamana ya Katiba na Sheria	Kutoa mwongozo wa kisheria kwa ajili ya maendeleo ya viwanda
21.	Wizara yenye dhamana ya Elimu	Kuandaa wahitimu wenye ujuzi kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
22.	Wizara yenye dhamana ya Sayansi na Teknolojia	Kuratibu masuala ya tafiti za kisayansi ili kuibua teknolojia kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
23.	Wizara yenye dhamana ya Afya	Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
24.	Wizara ya Maliasili na Utalii	Kuhakikisha upatikanaji wa malighafi zitokanazo na maliasili kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
25.	Wizara yenye dhamana ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	Kuhakikisha mazingira salama, kuunda teknolojia na kushiriki katika uendelezaji wa viwanda
26.	Wizara yenye dhamana ya Mambo ya Ndani ya Nchi	Kuhakikisha usalama wa nchi na kushiriki katika uendelezaji wa viwanda
27	Wizara yenye dhamana ya Habari, Utamaduni na Michezo	Kuhabarisha jamii kuhusu maendeleo ya viwanda nchini

Na.	Jina la Mdau	Wajibu na Majukumu
28	Wizara yenye dhamana ya Jinsia na makundi maalumu	Kutoa mwongozo na kuhamasisha ujumuishaji wa masuala ya jinsia na makundi maalumu katika shughuli za uendelezaji wa viwanda
29	Sekretarieti za Mikoa	Kuratibu shughuli za uendelezaji wa viwanda katika ngazi za mikoa
30	Mamlaka za Serikali za Mitaa	Kutenga na kuendeleza maeneo ya viwanda; na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za maendeleo ya viwanda na kuwekeza katika uendelezaji wa viwanda
31	Idara na Wakala za Serikali	Kutekeleza Sera katika maeneo yao ya mamlaka kwa kujumuisha shughuli za uendelezaji wa viwanda katika mipango, mikakati, na programu zao za maendeleo
32	Taasisi zilizo chini ya Wizara yenye dhamana ya viwanda	Kutekeleza Sera kulingana na majukumu yao ya kisheria
33	Washirika wa Maendeleo	Kushiriki katika kutekeleza Sera kwa kujenga uwezo wa kiufundi, kuchangia rasilimali fedha na teknolojia kwa maendeleo ya viwanda
34	Taasisi za elimu ya juu na utafiti	Kufanikisha utekelezaji wa Sera kwa kutoa: mafunzo; ubunifu; na utafiti kwa ajili ya uendelezaji wa viwanda
35	Sekta Binafsi	Utekelezaji wa Sera kwa kuwekeza katika uendelezaji wa viwanda
36	Asasi Zisizo za Serikali na Asasi za Kiraia	Kushiriki katika uendelezaji wa viwanda pamoja na kuhamasisha ushirikishwaji wa jamii katika maendeleo ya viwanda.
37	Mashirika ya Kikanda na Kimataifa	Kushiriki katika kutekeleza Sera kwa kujenga uwezo wa kiufundi na kuchangia rasilimali.
38	Vyombo vya habari	Kuandaa na kusambaza taarifa juu ya fursa za maendeleo ya viwanda zilizobainishwa katika Sera na utekelezaji wake.

5.3. MFUMO WA UFUATILIAJI NA TATHMINI

Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ni nyenzo muhimu ya kupitia na kutathmini utekelezaji wa Sera na kuhakikisha majukumu ya taasisi na wadau yanaratibiwa ipasavyo. Jukumu la ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji lipo chini ya wizara yenye dhamana ya viwanda kwa kushirikiana na wadau wengine. Kutokana na shughuli za sekta ya viwanda kuwa mtambuka, ushirikiano wa utekelezaji wa Sera unahitajika kutoka wizara zote za serikali, idara, wakala, mashirika, pamoja na mamlaka za serikali za mitaa. Aidha, kila mdau atakuwa na mfumo wa ufuatiliaji ulio wazi, wenye ufanisi na unaokidhi mahitaji ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 2025.

Katika kufuatilia utekelezaji wa Sera, kila mdau ataweka viashiria na vigezo vya kiutendaji, ukomo wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini; atapitia na kutathmini sera nyingine; na atapendekeza hatua zinazohitajika ili kufanya marekebisho. Aidha, kila mdau atafuatilia maendeleo ya utekelezaji wa malengo ya muda mfupi na muda mrefu, akitathmini shughuli zilizopangwa ikiwa zimetekelezwa kulingana na mpango. Mfumo huo unahakikisha kuwapo kwa utekelezaji madhubuti wa Sera na kufikiwa kwa malengo ya maendeleo ya viwanda.

5.4 HITIMISHO

Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 2025 imejikita katika kuanzisha viwanda vya kimkakati ambavyo ni muhimu kwa usalama wa taifa, ustawi wa kijamii na kiuchumi na maendeleo ya kiteknolojia ya nchi. Pamoja na hayo, toleo hili limezingatia kuwapo mfumo thabiti wa ufuatiliaji na tathmini unaoratibiwa na wizara yenye dhamana ya viwanda na kuwashirikisha wadau wakiwamo wizara zote za Serikali, idara, wakala, mashirika na mamlaka za serikali za mitaa. Vilevile, Sera imedadavua kwa utondoti maeneo yaliyoboreshwa kama vile masuala ya kisheria, masuala mtambuka, utafiti na ubunifu.

Sera hii imeweka msingi thabiti wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, inayoelekeza kuwa na uchumi jumuishi, shindani na endelevu unaoongozwa na viwanda na hatimaye kuongeza fursa za ajira nchini Tanzania, kuboresha maendeleo ya watu, kuchochea mageuzi ya kiuchumi, kuimarisha uhifadhi wa mazingira, kukuza uwezo wa viwanda, na kuimarisha viwanda mama.

Wizara ya Viwanda na Biashara, Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Viwanda, SLP 2996, 40478 Dodoma,
Tovuti: www.viwanda.go.tz